

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA
TANGAZO

LA

MAFUNDI UJENZI WA MAJENGO YA SHULE MPYA YA
SEKONDARI YA WASICHANA

27/07/2023

Halmashauri ya Wilaya ya Siha inapenda kutangaza nafasi za Kazi kwa Mafundi Ujenzi au kikundi kilichosajiliwa kwa kazi za ujenzi wa Majengo ya Shule mpya ya Sekondari ya Wasichana.

| SN | NAMBA YA ZABUNI | LOTI Na. | JINA LA ZABUNI |
|----|---------------------------------|----------|---|
| 1. | LGA/050/2023/2024/BW/F AC/07 | 1 | UJENZI WA VYUMBA 12 VYA MADARASA NA OFISI |
| 2. | LGA/050/2023/2024/BW/F AC/07 | 2 | UJENZI WA BWALO LA WANAFUNZI |
| 3. | LGA/050/2023/2024/BW/F AC/07 | 3 | UJENZI WA JENGO LA UTAWALA NA JENGO LA MATUNDU 16 YA VYOO |
| 4. | LGA/050/2023/2024/BW/F AC/07 | 4 | UJENZI WA MAJENGO YA MAABARA YA KEMIA,BIOLOJIA,FIZIKIA NA JIOGRAPHIA |
| 5. | LGA/050/2023/2024/BW/F AC/07 | 5 | UJENZI WA NYUMBA (2 in 1,YENYE VYUMBA 3 VYA KULALA,CHUMBA CHUMBA CHA WAGONJWA NA CHUMBA CHA JENERATOR |
| 6 | LGA/050/2023/2024/BW/F AC/07 | 6 | UJENZI WA BWENI LA WANAFUNZI 80STUDENT(8BLOCK) |

Sifa za Fundi Mjenzi

1. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri michoro ya aina yote ya ujenzi
2. Awe na elimu ya Form 1V/ujuzi wa kazi za ujenzi kwa kiwango Trade test na kuendelea. Kwa mwenye vyeti aambatanishe na atapewa kipaumbele.
3. Awe na uzoefu wa kufanya kazi katika majengo ya Serikali. Orodhesha angalau miradi mitatu (3) ya Serikali (Halmashauri) aliyokamilisha na mawasiliano ya taasisi husika
4. Awe hajawahi kuhukumiwa au kukutwa na hatia yoyote mahakamani.
5. Asiwe ameshindwa kukamilisha mradi wowote wa Serikali ndani na nje ya Halmashauri ya Wilaya.
6. Awe na akaunti ya Benki
7. Awe na Namba mlipa kodi (TIN)
8. Awe na mafundi wasaidizi wa fani husika wenye vyeti na vibarua wasiopungua kumi (10).
9. Awe na uwezo (kifedha) wa kuanza na kufanya kazi mpaka (15%) hatua ya kuweza kuomba malipo.

Masharti ya kazi za fundi

1. Fundi mjenzi anatakiwa kufika Ofisi ya Kitengo cha Ununuzi na Ugavi kwa ajili ya kuchukua nyaraka zinazohusiana na kazi hiyo ikiwa ni pamoja na kuchukua ramani na kujaza bei za kazi zote kwa kila hatua na kuweka viambatisho vyote husika kuanzia tatehe 27.07.2023. Kuanzia saa 2:30 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasili
2. Kila Fundi mjenzi anatakiwa kutembelea eneo la ujenzi kabla ya kurejesha barua ya maombi yake ili aweze kukagua eneo kabla ya kujaza bei.
3. Fundi anatakiwa kuomba Loti moja tu, Anaweza kuomba loti zaidi ya moja kwa kuambatanisha Ushaidi wa uwezo wa kifedha (Bank financial Statement) yenye balance isiyopungua 10,000,000.00. Pia atalazimika kuwasilisha dhamana au


koletero kutoka Taasisi yoyote ya kifedha inayotambulika na Serikali.

4. Malipo ya awali (advance payment) yatatolewa kwa muombaji atakaye timiza masharti kwa kuwasilisha dhamana kutoka Banki yoyote inayotambulika na Serikali na baada ya mwajili kupata uthibitisho kutoka benki husika.
5. Malipo yatafanyika baada ya kufanya tathmini (evaluation) na kutolewa hati ya malipo (Interim payment certificate) iliyoidhinishwa na Mhandisi wa Ujenzi toka Halmashauri ya Wilaya.
6. Fundi atalazimika kukatwa asilimia 10% ya fedha yote iliyopo katika mkataba wake kwa kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati kwa mujibu wa mkataba bila sababu za msingi.
7. Kazi zitatekelezwa katika kipindi cha miezi mitatu (3) siku 90 tu toka kusaini mkataba
8. Malipo yote yatakayofanyika yatakatwa makato yote ya kisheria yaani;-
 - i. Kodi ya zuio asilimia tano (5% withholding tax)
 - ii. Ushuru wa huduma (0.3% service levy)
 - iii. Fedha ya matazamio (5% Retention Money)
9. Kazi zote zitasimamiwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ambaye atakagua na kutathmini kazi kabla ya malipo hayajafanyika kupitia kamati za utekelezaji wa mradi.
10. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **02/08/2023** saa **04:00** asubuhi na maombi yote yatafunguliwa mbele ya waombaji watakaoamua kuhudhuria ufunguzi.

Ufunguzi utafanyika katika Ukumbi wa mikutano wa Halmashauri uliyopo ghorofa ya tatu.

11. Halmashauri ya Wilaya haitalazimika kumchagua fundi mjenzi mwenye bei ndogo kwa kuwa vigezo vyote vitazingatiwa.
12. Maombi yote yafungwe kwenye bahasha na yatumwe kwa,
Katibu wa Bodi ya Zabuni
Halmashuri ya Wilaya
S. L. P. 129 SIHA.
13. Nyaraka za kazi hizo zote pamoja na maelezo na ufafanuzi kuhusiana na kazi hizo yanapatikana katika ofisi ya kitengo cha Ununuzi na Ugavi Halmashauri ya Wilaya ya SIHA - Eneo la Dachcorner.

Tangazo limetolewa na,



Dr. Haji M. Mnasi

MKURUGENZI MTENDAJI (W)